ELIMU INAYOZINGATIA UMAHIRI

TATHMINI YA MWISHO WA MUHULA WA 3 2026

GREDI YA 6

KISWAHILI LUGHA

MUDA: **Dakika 40**

JINA: _____NAMBARI YA AD: _____

SHULE: _____TAREHE: _____

MAAGIZO KWA WANAFUNZI

1. Karatasi hii ina **maswali 30 ya kuchagua jibu sahihi**.
2. **Jibu maswali yote.**
3. Kwa kila swali, chagua **jibu sahihi kati ya machaguo manne A, B, C na D**.
4. **Andika herufi pekee ya jibu sahihi** katika nafasi uliyopewa.
5. Soma kila swali kwa makini kabla ya kujibu.
6. **Usiandike jibu zaidi ya moja** kwa swali lolote.

Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali ya 1 hadi 5.

(Safari na Rukia wananyunyuzia mimea maji.)

Safari: Masalkheri, Rukia?

Rukia: Akheri, Safari. Naona umeniwahi kufika leo.

Safari: *(Akitabasamu)* Nimefika muda mfupi tu uliopita, yapata nusu saa hivi.

Rukia: Nusu saa! Huo ni muda mfupi. Lazima umefaidi maonyesho mengi kabla sijafika.

Safari: Kipendacho moyo ni dawa. Ninayapenda maonyesho ya kitamaduni kwani hunipa fursa ya kipekee ya kujifunza tamaduni za wengine.

Rukia: Huo ni ukweli, ndugu yangu. Isitoshe, tukifurahia tamaduni za wenzetu tutawaelewa zaidi. Hii ni njia ya kuimarisha mshikamano wa kitaifa.

Safari: Naam. Hali kadhalika, mbali na kuiburudisha, uigizaji ni njia mojawapo ya kutambua na kukuza vipawa vyetu.

Rukia: *(Akitazama vijana walio jukwani)* Hilo linanikumbusha kwamba tulilipa kiingilio ili tupate nafasi hapa ukumbini. Haikosi waigizaji hawa watapata ujira wao kutokana na malipo hayo. Kwa hivyo, tamasha hizo kwa wengine ni njia ya kuumbua riziki.

Safari: Maigizo yenyewe huwa na dhamira mbalimbali, kuna vile kukashifu maovu, kuelimisha na kupinga mila potovu. Bila shaka, hii ni njia mwafaka ya kubadilisha jamii.

Rukia: Naona jukwaa liko tayari sasa. *(Anatulia kidogo.)* Na ni heri tukae ili tusipitwe na uhondo.

Safari: Sawa, dada yangu.

(Wanatulia kutazama mchezo jukwaani.)